
NATIONAL BUREAU OF STATISTICS
NBS
TANZANIA
STATISTICS FOR DEVELOPMENT

UHURU NA UMOJA

BANK OF TANZANIA

# RIPOTI YA UTAFITI WA WATALII WA KIMATAIFA WANAOONDOKA NCHINI, 2025
## MUHTASARI



# RIPOTI YA UTAFITI WA WATALII WA KIMATAIFA WANAOONDOKA NCHINI, 2025

## MUHTASARI

## Utangulizi

Sekta ya utalii duniani iliendelea kuimarika katika mwaka 2025, ambapo idadi ya watalii ilifikia bilioni 1.52, ikiwa ni ongezeko la asilimia 4 ikilinganishwa na mwaka 2024. Aidha, mapato ya utalii duniani yaliongezeka kwa asilimia 5 na kufikia dola za Marekani trilioni 1.9, yakichangiwa na kuongezeka kwa idadi ya watalii pamoja na matumizi ya wastani kwa kila mtalii.

Kwa Tanzania, sekta ilionesha mwenendo sawa na dunia katika uimara na ukuaji endelevu, na pia iliendelea kuwa miongoni mwa kichocheo muhimu cha mapato ya fedha za kigeni na maendeleo ya uchumi kwa ujumla. Sekta hii ilishuhudia ongezeko la idadi ya watalii kutoka nje sambamba na mapato yatokanayo na utalii, hali inayoakisi kuimarika baada ya kuathiriwa na janga la UVIKO-19 pamoja na migogoro ya kiuchumi inayoendelea duniani. Mwaka 2025, mapato ya utalii yaliongezeka kwa asilimia 13 kufikia dola za Marekani milioni 4,410.6 kutoka dola za Marekani milioni 3,903.1 mwaka 2024. Mafanikio haya yalichangiwa na ongezeko la idadi ya watalii pamoja na matumizi ya wastani kwa kila mtalii. Katika kipindi hicho, idadi ya watalii wa kimataifa iliongezeka kwa asilimia 6.7 kutoka watalii 2,141,895 mwaka 2024 hadi watalii 2,294,495 mwaka 2025.




*Katibu Mkuu, Wizara ya Maliasili na Utalii, Dkt. Hassan Abbasi, akipokea moja ya tuzo za World Travel Awards mwaka 2025, nchini Bahrain*

Utendaji huu mzuri uliimarishwa zaidi na mafanikio mbalimbali ya sekta ya utalii mwaka 2025. Katika kipindi hicho, Tanzania ilipata tuzo za “World Travel Awards”, ikiwemo kuwa mwenyeji wa hafla ya 32 ya Afrika na Bahari ya Hindi, huku Hifadhi ya Taifa ya Serengeti ikitajwa kuwa hifadhi bora zaidi duniani. Aidha, Hifadhi ya Taifa Tanzania (TANAPA) ilipokea tuzo ya



*Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Chana katika hafla ya ufunguzi wa Tuzo za 32 za World Travel Awards (WTA) kwa Kanda ya Afrika na Bahari ya Hindi, iliyofanyika katika Hoteli ya Johari Rotana, Dar es Salaam.*

“European Quality Choice Diamond” kwa ubora wa utoaji huduma, na Tanzania kushika nafasi ya nne duniani kwa uzuri wa asili. Vilevile, nchi iliandaa Jukwaa la Pili la Kikanda la Utalii wa Vyakula Afrika pamoja na safari maalum ya kidiplomasia, hatua zilizoongeza utambulisho wa kimataifa wa vivutio vya utalii vya Tanzania.

Kutokana na umuhimu wa sekta ya utalii katika uchumi wa nchi, Wizara ya Maliasili na Utalii (MNRT), Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Idara ya Uhamiaji, na Kamisheni ya Utalii Zanzibar (ZCT), zilifanya utafiti wa 25 wa watalii wa kimataifa wanaoondoka nchini mwaka 2025. Utafiti huu unakusanya taarifa kuhusu matumizi ya watalii, ambazo ni muhimu katika kukadiria mapato ya utalii yanayotumika katika utayarishaji wa Takwimu za Mizania ya Malipo (BOP). Pia, taarifa hizi hutoa mwongozo muhimu kwa sera za serikali na maamuzi ya kibiashara kwa sekta binafsi.

## Madhumuni

Madhumini ya utafiti huu ni kutoa takwimu sahihi kuhusu tabia, matumizi na mienendo ya watalii wa kimataifa. Taarifa hizi ni muhimu kwa mipango ya maendeleo, uandaaji wa takwimu za kitaifa, pamoja na kukuza utalii na uwekezaji.

## Eneo la Utafiti


Katika kufikia madhumini haya, utafiti wa mwaka 2025 ulifanyika katika vituo nane vikuu vya kuondokea wageni: Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (AAKIA), Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), pamoja na mipaka ya Horohoro, Namanga, Tunduma, Mtukula na Manyovu. Maeneo haya ni vituo vikuu vinavyotumiwa na wageni wa kimataifa wanaoondoka nchini. Muda wa utafiti ulikuwa wa kipindi cha wiki mbili kuanzia tarehe 11 hadi 24 Agosti 2025, ambapo jumla ya wahojiwa 10,309 walishiriki, wakiiwakilisha wageni 22,838 waliokuwa wakiondoka nchini.

# Matokeo muhimu ya utafiti

## Utalii wa Dunia waendelea kuimarika mwaka 2025

Idadi ya watalii wa kimataifa duniani ulifikia bilioni 1.52 mwaka 2025, ikiwa ni ongezeko la takribani watalii milioni 60 ikilinganishwa na mwaka 2024, sawa na ukuaji wa asilimia 4 kwa mwaka. Ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa mahitaji ya utalii, kuongezeka kwa miundombinu ya usafiri wa anga, urahisishaji wa viza, pamoja na kuendelea kuimarika kwa sekta ya utalii katika maeneo ya Asia na Pasifiki Kikanda, Ulaya iliendelea kuwa eneo linaloongoza kwa idadi ya watalii, likichangia zaidi ya nusu ya watalii wote waliosafiri duniani, huku Mashariki ya Kati ikirekodi ukuaji mkubwa zaidi, na Afrika pamoja na Ulaya yalivuka viwango vya mwaka 2019 kabla ya UVIKO-19, hali iliyochangiwa na kuboreshwa kwa usafiri wa anga, kurahisishwa kwa masharti ya usafiri, na kuongezeka kwa mahitaji ya utalii wa utamaduni na asili. Aidha, mapato ya utalii duniani yaliendelea kuongezeka, nakufikia dola za Marekani trilioni 1.9 mwaka 2025, sawa na ongezeko la asilimia 5 kutoka dola za Marekani trilioni 1.7 mwaka 2024 (Kielelezo Na 1).

**Kielelezo Na 1: Idadi ya Watalii wa Kimataifa na Mapato ya Utalii Duniani, 2019-2025**





Chanzo: UNWTO Barometer, Januari 2026

Tanzania iliendelea kufuata mwenendo wa dunia kwa sekta ya utalii kuendelea kuimarika mwaka 2025, ikichangiwa na ongezeko la watalii pamoja na mapato. Idadi ya watalii iliongezeka kutoka 2,141,895 mwaka 2024 hadi 2,294,495 mwaka 2025, sawa na ukuaji wa asilimia 6.7, huku mapato ya utalii yakifikia kiwango cha juu cha dola za Marekani milioni 4,410.6 kutoka dola za Marekani milioni 3,903.1 mwaka 2024. Ukuaji huu unaakisi mahitaji endelevu ya kimataifa, kuboreshwa kwa usafiri wa anga, na ongezeko la matumizi kwa kila mtalii, huku sekta ikiendelea kufanya vizuri zaidi ya viwango vya kabla ya janga la UVIKO-19 (Kielelezo Na 2).

**Kielelezo Na 2: Idadi ya watalii wa kimataifa Tanzania, 2015 - 2025**

*Milioni*




Chanzo: Idara ya Uhamiaji


## Masoko Makuu ya Utalii yaendelea kuongoza kwa ongezeko la watalii

Matokeo ya utafiti wa mwaka 2025 yanaonesha kuwa masoko ya asilia ya watalii yaliendelea kubaki yaleyale. Kwa Tanzania , Marekani iliongoza, ikifuatiwa na Italia na Ufaransa, huku Zanzibar ikiendelea kuongozwa na Italia, ikifuatiwa na Ufaransa na Uingereza. Masoko 15 bora yalichangia asilimia 75 ya watalii wote Tanzania na asilimia 77 kwa Zanzibar.Kwa kiasi kikubwa, mapato haya hayajabadilika kutoka mwaka 2024, isipokuwa

kwa mabadiliko madogo yakijitokeza ambapo Uholanzi na India ziliingia katika orodha, zikichukua nafasi ya Australia na Burundi, hali inayoonesha kuongezeka kwa masoko mapya kutokana na juhudi zilizofanywa za kukuza utalii Kielelezo Na. 3 na 4).


### Kielelezo Na 3: Masoko makuu 15 ya Watalii kwa URT

*Asilimia*




### Kielelezo Na 4: Masoko makuu 15 ya Watalii kwa Zanzibar

*Asilimia*



### Watalii wenye umri wa Miaka 25–44 waliendelea kuongoza


Aidha, watalii wenye umri wa miaka 25–44 walichangia karibu nusu ya watalii wote, wakifuatiwa na wenye miaka 45–64, kwa Tanzania pamoja na Zanzibar. Masoko makuu kwa watalii wenye miaka 25–44 yaliendelea kuwa Italia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, China na Uganda, watalii wenye umri wa miaka 65 na zaidi wakionekana zaidi kutoka Marekani na India. Zanzibar pia ilionesha mwenendo huo huo, huku watalii wenye miaka 25–44 wakiongoza, wakifuatiwa na masoko mengi yalionesha kuwa na watu walio katika umri wa kufanya kazi, isipokua kwa masoko ya Marekani, Australia na Canada, ambayo yalikuwa na watalii wengi wenye umri wa miaka 65 na zaidi..

### Watalii wengi walitembelea Tanzania kwa ajili ya Mapumziko na Likizo

Watalii wengi walitembelea Tanzania mwaka 2025 kwa ajili ya mapumziko na likizo, ambapo ilichangia asilimia 64.6 kwa Tanzania  na asilimia 92.9 kwa Zanzibar. Mwenendo huu umekuwa ukijitokeza hata miaka ya nyuma ikifuatiwa na kutembelea ndugu na marafiki pamoja na biashara. Aidha, watalii wa mapumziko walivutiwa zaidi na vivutio vya wanyamapori na fukwe, wengi wao wakitoka Marekani, Italia na Ufaransa. Watalii waliokuja kutembelea ndugu wakitoka zaidi nchi jirani hususani Kenya na Burundi, na watalii wa biashara wakitoka zaidi Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, hali hii ikiashiria nafasi ya Tanzania kama kitovu cha shughuli za kikanda..

**Kielelezo Na. 5: Mchanganuo wa watalii kwa madhumuni ya safari**

*Asilimia*





## Mpango wa safari wa kifurushi umeendelea kuwa kinara kwa watalii

Mpango wa safari kwa kifurushi uliendelea kutumiwa zaidi na watalii kwa Tanzania na Zanzibar, mwaka 2025. Tanzania , asilimia 58.8 ya watalii walitumia mpango wa safari kwaa kifurushi ikilinganishwa na asilimia 56.3 mwaka 2024, ambapo watalii wa masoko ya mbali kama Marekani, Israel na Poland walionekana kupendelea zaidi mpango huu. Hata hivyo, watalii kutoka nchi jirani kama Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya na Uganda walipendelea zaidi mpango wa safari usio wa kifurushi. Ongezeko hilo pia lilionekana Zanzibar, ambapo watalii waliotumia mpango wa safari kwa kifurushi walifikia asilimia 67.2 kutoka asilimia 61.8 mwaka 2024, huku masoko kama Uholanzi, Italia na Ufaransa yakiongoza. Aidha, watalii wa mapumziko walipendelea zaidi mpango wa safari kwa kifurushi, wakati wale

waliokuja kwa ajili ya biashara, shughuli za kujitolea na kutembelea ndugu walipendelea safari zisizo za kifurushi kutokana na urahisi wa kupanga safari zao wenyewe (Kielelezo Na. 6 na 7).


**Kielelezo Na  6: Mwenendo wa mipango ya safari kwa watalii, URT**

*Asilimia*




**Kielelezo Na  7: Mwenendo wa mipango ya safari kwa watalii, Zanzibar**

*Asilimia*



## Muda wa kutalii nchini umeendelea kuwa wa wastani

Mwaka 2025, muda wa wastani wa kukaa ulikuwa siku 9 Tanzania, ukipungua kutoka siku 10 mwaka 2024. Kwa Zanzibar, wastani wa muda wa kukaa ulikuwa siku 6, ukipungua kutoka siku 7 mwaka 2024. Kwa upande wa Tanzania, watalii kutoka Uholanzi walikaa muda mrefu zaidi (siku 15), wakifuatiwa na wale kutoka Ujerumani, Uingereza na Hispania. Kwa Zanzibar, watalii waliokaa muda mrefu zaidi walitoka Ufaransa, Ujerumani, Uholanzi, China, Poland na Italia, kwa wastani wa siku 8 kwa kila nchi. Kwa ujumla, watalii wa mapumziko walikaa muda mrefu zaidi kuliko watalii waliokuja kwa ajili ya biashara (Kielelezo Na. 8).

**Kielelezo Na 8: Wastani wa Muda wa Kukaa wa Masoko 15 Makuu ya Watalii kwa Madhumuni ya Ziara, URT na Zanzibar**

URT

| | Dhumuni la safari | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Uraia | Likizo na Mapumziko | Biashara | Kutembelea Marafiki na Jamaa | Nyingine | Wastani |
| Marekani | 10 | 10 | 10 | 12 | 11 |
| Italia | 10 | 5 | 11 | 14 | 10 |
| Ufaransa | 11 | 8 | 13 | 16 | 12 |
| Kenya | 5 | 6 | 8 | 13 | 8 |
| Uingereza | 12 | 7 | 14 | 18 | 13 |
| Ujerumani | 13 | 7 | 18 | 14 | 13 |
| Zambia | 6 | 11 | 9 | 6 | 8 |
| Uholanzi | 15 | 8 | 15 | 20 | 14 |
| Hispania | 10 | 6 | 18 | 19 | 13 |
| DRC | 14 | 9 | 9 | 23 | 14 |
| China | 7 | 9 | 9 | 39 | 16 |
| Afrika Kusini | 7 | 6 | 10 | 6 | 7 |
| India | 7 | 16 | 10 | 3 | 9 |
| Canada | 10 | 20 | 13 | - | 14 |
| Zimbabwe | 7 | 4 | 5 | 4 | 5 |
| Wastani | 10 | 9 | 11 | 15 | 11 |


| | | | | | Zanzibar |
|---|---|---|---|---|---|
| | Dhumuni la safari | | | | |
| Uraia | Likizo na Mapumziko | Biashara | Kutembelea Marafiki na Jamaa | Nyingine | Wastani |
| Italia | 7 | - | 7 | 6 | 7 |
| Ufaransa | 7 | 2 | 8 | 13 | 8 |
| Uingereza | 7 | 3 | 7 | 6 | 6 |
| Marekani | 5 | 5 | 6 | 8 | 6 |
| Ujerumani | 7 | 10 | 8 | 8 | 8 |
| Uholanzi | 7 | - | 7 | 10 | 8 |
| Hispania | 6 | 1 | 10 | - | 6 |
| Afrika Kusini | 7 | 4 | 10 | 5 | 6 |
| Australia | 5 | - | 6 | 4 | 5 |
| Polandi | 8 | 10 | 7 | - | 8 |
| Kenya | 4 | 5 | 5 | 2 | 4 |
| Ubelgiji | 7 | - | 12 | 2 | 7 |
| Canada | 5 | 9 | 5 | 5 | 6 |
| Ugiriki | 6 | - | - | - | 6 |
| Austria | 7 | 6 | - | 22 | 12 |
| Wastani | 6 | 6 | 8 | 7 | 7 |

## Watalii wa mara ya kwanza wameendelea kuongezeka

Mwaka 2025, watalii wa mara ya kwanza waliendelea kuwa wengi katika Tanzania na Zanzibar, huku Zanzibar ikirekodi zaidi ya asilimia 78 ya watalii wa aina hiyo. Watalii wa mara ya kwanza walitoka zaidi katika masoko ya mbali kama Hispania, Marekani, Uholanzi, Ujerumani na Italia, wakati wanaorudia walitoka zaidi katika nchi jirani kama Kenya, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Zimbabwe. Watalii wa mara ya kwanza walipendelea zaidi mpango wa safari kwaa kifurushi kutokana na urahisi wake, wakati wanaorudia walipendelea safari zisizo za kifurushi kutokana na uzoefu na uelewa wao wa mazingira.

**Kielelezo Na 9: Watalii wa mara ya kwanza na waliowahi kutembelea, URT na Zanzibar**

*Asilimia*




## Ubora wa utalii Tanzania umeongeza matumizi na mapato ya utalii

Watalii waliendelea kuridhishwa na uzoefu wao nchini Tanzania, ambapo ukarimu wa Watanzania, uzuri wa mazingira, wanyamapori na vyakula vya asili vilitajwa kuwa vivutio vikuu. Aidha, maboresho ya huduma za utalii na juhudi za uhifadhi wa rasilimali za asili yaliendelea kuongeza mvuto wa Tanzania, huku mtandao na mitandao ya kijamii vikijitokeza kama vyanzo muhimu vya taarifa kuhusu vivutio vya utalii nchini.

Kuridhika huku kwa watalii kulichangia kuongezeka kwa matumizi yao wakati wa ziara. Mwaka 2025, wastani wa matumizi kwa mtalii kwa usiku ulifikia dola za Marekani 289 Tanzania Bara na dola za Marekani 274 Zanzibar, ambapo watalii waliotumia mpangilio wa safari kwa kifurushi walitumia zaidi kuliko wale waliotumia safari zisizo za kifurushi. Watalii kutoka China waliongoza kwa kiwango cha matumizi, wakifuatiwa na wale kutoka Italia, Uingereza, Ujerumani, Marekani na India. Aidha, watalii walioshiriki uwindaji, utalii wa utamaduni, safari za wanyamapori na kupanda milima walirekodi matumizi makubwa zaidi.

## Mapato ya utalii yaendelea kuongezeka

Mapato ya utalii yameendelea kuongeza na kwa mwaka 2025, yaliongezeka kwa asilimia 13 na kufikia dola za Marekani milioni 4,410.6, yakichangiwa na ongezeko la watalii na wastani wa matumizi kwa mtalii. Watalii waliokuja kwa ajili ya likizo na mapumziko walichangia sehemu kubwa ya mapato hayo, huku watumiaji wa safari za kifurushi wakichangia zaidi ya robo tatu ya mapato yote. kwa Zanzibar, mapato ya utalii yaliongezeka kwa asilimia 19.3, kufikia dola za Marekani milioni 1,190.8, kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watalii wa kimataifa. Watalii wa mapumziko na likizo waliendelea kuwa chanzo kikuu cha mapato ya utalii visiwani.

## Kielelezo Na 10: Mapato ya utalii kwa aina ya mpangilio wa safari na madhumuni ya ziara, Tanzania

*Dola za Marekani Milioni*

| Madhumuni ya safari | Mpango wa safari | | Mapato |
|---|---|---|---|
| | Kifurushi | Bila Kifurushi | |
| Biashara | 1.3 | 41.0 | 42.2 |
| Likizo na Mapumziko | 3,303.9 | 929.7 | 4,233.5 |
| Kutembelea Marafiki na Jamaa | 3.7 | 77.3 | 81.0 |
| Nyingine | 9.2 | 44.7 | 53.9 |
| Mapato ya Utalii | 3,318.0 | 1,092.6 | 4,410.6 |

## Kielelezo Na 11: Mapato ya utalii kwa aina ya mpangilio wa safari na madhumuni ya ziara, Zanzibar

*Dola za Marekani Milioni*

| Madhumuni ya safari | Mpango wa safari | | Mapato |
|---|---|---|---|
| | Kifurushi | Bila Kifurushi | |
| Biashara | 0.2 | 0.0 | 0.3 |
| Likizo na Mapumziko | 702.6 | 486.4 | 1,188.9 |
| Kutembelea Marafiki na Jamaa | 0.4 | 1.1 | 1.5 |
| Nyingine | 0.0 | 0.1 | 0.1 |
| Mapato ya Utalii | 703.2 | 487.6 | 1,190.8 |

## Vivutio vikuu vya utalii vinaendelea kuongoza katika kuvutia watalii

Watalii nchini Tanzania walijihusisha zaidi na safari za wanyamapori, mapumziko ya fukweni, kutembelea ndugu na marafiki, pamoja na shughuli za biashara. Vivutio vilivyoongoza ni pamoja na Ngorongoro, Serengeti, fukwe, Stone Town na Tarangire, ambavyo vilichangia takribani asilimia 59 ya watalii mwaka 2025, kutoka asilimia 62.6 mwaka 2024. Hali hii ikiashiria kuongezeka kwa watalii wanaotembelea maeneo mengine mapya. Watalii wa wanyamapori, kupanda milima na uwindaji walipendelea mpango wa safari kwa kifurushi, huku wale wa biashara na kutembelea ndugu wakipendelea safari zisizo za kifurushi.

Kwa ujumla, matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa Tanzania imeendelea kuimarisha nafasi yake kama moja ya maeneo yanayovutia watalii duniani. Kuongezeka kwa idadi ya watalii, mapato ya utalii, pamoja na kuongezeka kwa ubora wa vivutio mbalimbali, kunaonesha mafanikio ya juhudi za kukuza utalii na kupanua wigo wa bidhaa za utalii nchini. Mwenendo huu unatarajiwa kuendelea kuimarisha mchango wa sekta ya utalii katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Taifa.



MINISTRY OF NATURAL RESOURCES AND TOURISM
WWW.MALIASILI.GO.TZ

BANK OF TANZANIA (BOT)
WWW.BOT.GO.TZ

ZANZIBAR COMMISSION FOR TOURISM (ZCT)
WWW.ZANZIBARTOURISM.NET

NATIONAL BUREAU OF STATISTICS (NBS)
WWW.NBS.GO.TZ

IMMIGRATION SERVICES DEPARTMENT
WWW.MOHA.GO.TZ